AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

BARAZA KUU
Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Nne
15 Januari - 15 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

EX.CL/1463(XLIV)
Lugha Chanzi: kiingereza

RIPOTI YA KAMATI NDOGO KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, DEMOKRASIA NA UTAWALA (HRDG)

I. UTANGULIZI

1. Kamati Ndogo ya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) kuhusu Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala (HRDG) ilifanya shughuli mbalimbali mwaka 2023. Muhtasari wa shughuli hizi unajumuisha shughuli zifuatayo ;

a. Ilikamilisha Mpango Kazi wa mwaka 2023 wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG;
b. Ilithibitisha Ripoti ya Utawala wa Afrika;
c. Mkutano wa pili na Baraza la Amani na Usalama, uliofanyika kwa pamoja na Jukwaa la Utawala wa Afrika;
d. Kikazi Kazi cha Pamoja kati ya Kamati Ndogo na ACHPR.
e. Ilipokea taarifa kutoka kwa :
   i. Tume ya Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR);
   ii. Baraza la Uchumi, Jamii na Utamaduni (ECOSOCC);
   iii. Kurugenzi ya Utawala na Uzuiaji wa Migogoro (GCPD) - Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (PAPS) juu ya Kitengo cha Katiba na Utawala wa Sheria;
   iv. Mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Jukwaa la Utawala wa Afrika (AGP).

2. Ripoti inatoa muhtasari wa shughuli za Kamati Ndogo kuhusu HRDG kwa maeneo yaliyoorodheshwa hapo juu zinazoanzia **Januari hadi Desemba 2023**

II. MAFANIKIO YA KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU HRDG KWA MWAKA 2023

WASILISHO NA UPITISHAJI WA RASIMU YA MPANGO KAZI WA MWAKA 2023 WA KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU HRDG

3. Kufuatia mkutano wa kwanza kwa njia ya mtandao wa Kamati Ndogo, ambapo wajumbe walijadili na kufanya marekebisho kwenye Rasimu ya mpango kazi wa mwaka 2023, rasimu hiyo ya mpango kazi ilitumwa kwa Wajumbe wa Kamati Ndogo ya PRC na kisha kupitishwa pamoja na marekebisho yake.

UTHIBITISHAJI WA RIPOTI YA UTAWALA WA AFRIKA (AGR-23) UNAOFANYWA NA KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, DEMOKRASIA NA UTAWALA NA AMANI NA USALAMA – JANUARI 2023

4. Mpango wa Kujitathmini Kiutawala bora barani Afrika (APRM) ilifanya mkutano wa kuthibitisha ripoti ya Ripoti ya Utawala wa Afrika ya mwaka 2023 (AGR-23) na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na Kamati ya Wataalamu ya Baraza la Amani na Usalama, kuanzia tarehe 13 hadi 14 Januari 2023, mjini Djibouti, Jamhuri ya Djibouti. Mkutano ulitoa fursa ya kupokea mrejesho kutoka Nchi Wanachama juu ya rasimu ya AGR-23.

5. AGR-23 ilishughulikia suala muhimu la Mabadiliko ya Serikali yasiyo ya Kikatiba (UCG) barani Afrika. Kwa kujikita kwenye uchambuzi wa kina, ripoti ilikusanya matokeo kutoka vyanzo tofauti tofauti kumi na tatu. Vyanzo hivi vilijumuisha ripoti sita za nchi mahsusi zinazochunguza mafunzo yaliyopatikana kutokana na uzoefu uliopita wa UCG, ripoti tano za kimaudhui zinazochunguza vichocheo na visababishi vya UCG, na ripoti mbili za mashauriano zinazotathmini kufaa kwa mifumo ya kawaida na mifumo ya adhabu katika kushughulikia matukio ya UCG.

6. AGR-23 baadaye ilipitishwa kwa mafanikio na Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mnamo Februari 2023.

MKUTANO WA PILI NA BARAZA LA AMANI NA USALAMA, ULIOFANYIKA KWA PAMOJA NA JUKWAA LA UTAWALA WA AFRIKA

7. Kwa kuzingatia mikutano ya awali ya kubadilishana uzoefu na Kamati Ndogo na AGP mnamo tarehe 1 Agosti 2022 na 11 Agosti 2022, mtawalia, Baraza la Amani na Usalama (PSC) limeazimia kurasimisha na kuratibu mazungumzo hayo kila mwaka.

8. Ili kutekeleza uamuzi huu, PSC, chini ya Uongozi wa Jamhuri ya Burundi, iliitisha mkutano kwa njia ya mtandao uliojikita kwenye kaulimbiu: “Mkutano na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Haki za Binadamu, demokrasia na Utawala (HRDG), na Jukwaa la Muundo wa Utawala wa Afrika (AGP), mnamo tarehe 11 Agosti 2023. Mkutano huu ulitoa jukwaa lenye thamani kwa ajili ya kuimarisha zaidi ubia na kubadilishana uzoefu mzuri katika kufikia malengo ya pamoja.

9. Mikutano ya pamoja ililenga kukuza na kuimarisha demokrasia, utawala bora na utawala wa sheria. Kwa kuzingatia matokeo ya mikutano iliyotangulia, PSC ilisisitiza umuhimu wa Nchi zote Wanachama kufuata kikamilifu vipengele vya Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Chaguzi, na Utawala (ACDEG). Msisitizo huu unaendana na kanuni za msingi zilizo kwenye Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika (*Constitutive Act*) (Ibara ya 3 na 4) na Itifaki Inayohusiana na Uanzishwaji wa Baraza la Amani na Usalama (Ibara za 3(f) na 7(m)), ambayo inasisitiza uhusiano wa utawala wa kidemokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu, na uzuiaji wa migogoro.

10. Zaidi ya hayo, mikutano hiyo ilisaidia kuimarisha ushirikiano na jitihada za ushirikiano kati ya taasisi na vyombo mbalimbali vya AU, pamoja na kati ya AU na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Vyombo vya Kikanda vya Ulinzi wa Haki (RECs/RMs). Mbinu hii ya ushirikiano ni muhimu katika kufanikisha amani, usalama, utulivu, na maendeleo ya kudumu barani Afrika.

11. PSC ilisisitiza umuhimu wa ushirikiano ulioimarishwa kati ya PSC na Kamati Ndogo, pamoja na AGP kwa kupitisha mipango inayolenga kukuza utawala wa kidemokrasia na utulivu barani Afrika pamoja na mbinu za jumla na za pande nyingi zinazojikita kwenye uhusiano kati ya amani, usalama na maendeleo. Kwa mujibu wa taarifa ya mkutano wa 1167 wa PSC uliofanyika tarehe 11 Agosti 2023, PSC miongoni mwa mambo mengine:

a) Ilithibitisha tena umuhimu wa ahadi ya Nchi Wanachama kwenye uridhiaji, uingizaji kwenye mipango ya ndani, utekelezaji, na utoaji ripoti wa wote kuhusu Maadili ya Pamoja ya AU, hususan Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Chaguzi, na Utawala (ACDEG). Kuhusiana na hili, Baraza lilizihimiza Nchi Wanachama ambazo bado hazijasaini, hazijaridhia, na hazijaingiza kwenye mipango ya ndani Mkataba huo;

b) Ilisisitiza umuhimu wa kuimarisha mara kwa mara uwezo wa kitaasisi wa Nchi Wanachama, kwa kujenga mifumo thabiti ya utawala kwa ajili ya uzuiaji, tahadhari ya mapema na hatua ya mapema; kuimarisha muundo wa utawala wa bara, muundo wa amani na usalama na kuunda mahusiano ya kazi kati ya Vyombo, RECs na Umoja wa Afrika kwa ajili ya ubora; kushirikisha raia vizuri kwa kutoa umakini maalumu kwa vijana, wanawake na makundi yaliyo hatarini; na kuanzisha ubia unaojikita kwenye maarifa;

c) Ilitambua mchango mkubwa wa Jukwaa la AGA katika kukuza utawala wa kidemokrasia, amani na usalama katika Bara, pamoja na kuimarisha utangamano wa karibu kati ya Muundo wa Amani na Usalama wa Afrika (APSA) na Muundo wa Utawala wa Afrika (AGA);

d) Iliiomba Tume kuharakisha utekelezaji wa kituo cha utawala Afrika *African Governance Facility*, ili kuwezesha ukusanyaji bora wa rasilimali kwa ajili ya kusaidia mipango ya AGP na Nchi Wanachama katika kukuza utawala bora na kuimarisha demokrasia ndani ya Bara; na katika muktadha huohuo, pia iliiomba Tume ya AU kuimarisha zaidi Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na AGP, pamoja na uwezo wa kitaasisi wa Sekretarieti ya AGA-APSA ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi;

e) Ilisisitiza haja ya kuwa na ushirikiano imara na ukamilishano wa jitihada kati ya na miongoni mwa AGA na APSA, Baraza na Kamati Ndogo ya PRC, Jukwaa la Utawala wa Afrika, huku zikiheshimu mamlaka husika ya kila mmoja wao; Ilitoa wito kwa wajumbe wa Jukwaa la AGA na Ofisi (*Bureau*) kushirikisha PSC kwenye kazi ya Jukwaa ili kuendelea kuwezesha ushirikiano wao wa kimashauriano unaolenga kubadilisha ajenda ya utawala wa kidemokrasia na ulio bora kuwa matokeo yanayoonekana;

f) Ilisisitiza haja ya Mwenyekiti wa PSC wa Mwezi na Sekretarieti ya PSC kushiriki kikamilifu zaidi kwenye mikutano ya wadau ya Jukwaa la Utawala wa Afrika kila mwaka;

g) Iliomba Tume ya AU, Jukwaa la Utawala wa Afrika na Sekretarieti ya AGA-APSA kuandaa mkutano wa pamoja wa mashauriano ili kutambua mipango ya pamoja zaidi ya vikao vya kubadilishana uzoefu, kwa kutoa umakini maalumu kwenye maeneo yafuatayo;

- Ziara za ukuzaji za Pamoja za PSC, Kamati Ndogo ya PRC na AGP juu ya vyombo vya AU vya maadili ya pamoja; zilitoa wito wa kushiriki zaidi katika diplomasia ya kuzuia migogoro na jitihada za usuluhishi;

- Ushiriki wa PSC katika upangaji na utoaji wa Mipango Mikubwa ya AGA na uanzishwaji wa vyombo vya ufuatiliaji wa maamuzi ya kikao cha pamoja kati ya PSC na AGP.

KIKAO KAZI CHA PAMOJA KATI YA KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU HRDG NA ACHPR

12. Kwa mujibu wa mpango kazi ulioanzishwa kwa ajili ya mwaka 2023, Kikao Kazi cha Pamoja kiliitishwa kati ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na ACHPR kuanzia tarehe 5 hadi 7 Desemba 2023, mjini Dakar Senegal. Kikao Kazi cha Pamoja kilisaidia kuimarisha ushirikiano kati ya ACHPR na Kamati Ndogo ya PRC, na pamoja na kuwa na jukumu muhimu katika kuwezesha mbinu iliyoratibiwa na imara katika kulinda na kukuza haki za binadamu na watu. Ofisi za Kamati Ndogo za PRC kuhusu Usimamizi na Uratibu wa Jumla juu ya Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala (GSCBFAM) na juu ya Masuala ya Muundo pia zilishiriki kwenye Kikao Kazi cha Pamoja katika majadiliano shirikishi yanayolenga kuboresha utendaji wa ACHPR, kutetea rasilimali zake za kutosha za uwezo wa kibinadamu na kifedha katika muktadha wa utekelezaji wa mageuzi ya AU.

13. Kikao Kazi cha Pamoja kilionekana kuwa ni cha muhimu katika kuimarisha maelewano kati ya Kamati Ndogo na ACHPR kuhusiana na mamlaka yao husika, taratibu, na faida linganishi. Uelewa huu ulioimarishwa ulitoa njia ya kuainisha fursa za jitihada shirikishi na uimarishaji wa pande zote katika kufikia malengo yaliyomo kwenye Ajenda 2063.

14. Kikao Kazi kilikubaliana juu ya mikakati madhubuti na ahadi za ACHPR na mpango wa ushirikiano imara na uhusiano kati ya ACHPR na Kamati ndogo ya PRC kuhusu HRDG, kama ilivyokubaliwa na wote, zikiwemo ahadi za msaada muhimu wa Kamati ndogo ya Mageuzi ya Kimuundo na GSCBFAM, katika kuimarisha na kulinda haki za binadamu ndani ya bara.

15. Kikao Kazi cha Pamoja kilipitisha **mapendekezo yafuatayo kwa Nchi wanachama** :

i. Kuunga mkono kauli mbiu ya AU iliyopendekezwa ya mwaka 2025 kama "*Mwaka wa Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala*";
ii. Kutoa rasilimali za kiufundi na kifedha kwa ACHPR ndani ya vigezo vilivyokubaliwa na kwa kupitia mchakato sahihi, ikiwemo kwa mujibu wa **EX.CL/329(XI) Rev.1**, wa Mkutano wa Kawaida wa 11 wa Baraza Kuu, ambao ulifanyika kuanzia tarehe **25 hadi 29 Juni 2017** kuhusu Ripoti juu ya Uoanishaji wa Sera ya Malipo;
iii. kuendelea kutetea vyombo vya Sera vya AU kuongeza bajeti ya ACHPR ili itekeleze mamlaka yake ipasavyo; Kuimarisha ACHPR katika kazi yake ya

kushughulikia masuala ya haki za binadamu ndani ya bara ili kukuza utekelezaji wa wajibu wa kisheria;

iv. Kuhimiza utekelezaji wa maamuzi/ mapendekezo ya ACHPR, kama yanavyoweza kutumika kwenye Nchi;

v. Kuzingatia kuazima wafanyakazi kwenye ACHPR na kuhimiza uhuishaji wa mikataba ya wafanyakazi ya muda mfupi ili kuziba pengo lake la sasa la wafanyakazi, kwa kuendana na Sheria na kanuni za Wafanyakazi;

vi. Ilihimizwa kuridhia vyombo vya haki za binadamu chini ya uangalizi wa ACHPR; na

vii. Kualika Nchi Wanachama kuwasilisha ripoti zao za mara kwa mara kwa ACHPR kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika na vyombo husika vya haki za binadamu.

16. Kikao Kazi cha Pamoja kilipitisha **Mapendekezo ya Jumla yafuatayo kwa ACHPR:**

i. Kuhakikisha kukutana kila mwaka kwa Kikao Kazi kati ya ACHPR na PRC kwa mujibu wa Maamuzi **EX.CL/Dec.995 (XXXII),** ya 2018 na **EX.CL/Dec.1045 (XXXIV)** ya 2019, na pale kinapokutana kwa kutegemea upatikanaji wa rasilimali, kuepuka vipindi ambavyo watu wana shughuli nyingi (*peak periods*) ili kuhakikisha ushiriki kamili;

ii. Kuanzisha uhusiano wa kishirikiano na Kamati Maalumu ya Kiufundi ya AU inayohusika na Haki na Masuala ya Kisheria ili kufuatilia na kukuza Itifaki muhimu za haki za binadamu za Afrika;

iii. Kufanya uchambuzi wa uzoefu mzuri na changamoto za Nchi Wanachama kuhusiana na utekelezaji wa maamuzi na mapendekezo ya ACHPR, na kutoa matokeo ya uchambuzi kwa Nchi Wanachama;

iv. Kuweka mipango ya kina ya kujenga uwezo na Nchi Wanachama ili kuimarisha uelewa mzuri wa taratibu zake za kazi, kuimarisha mahusiano na Nchi wanachama, na kukuza utekelezaji wa maamuzi yake;

v. Kuunda mahusiano yaliyowiana na imara kati ya ACHPR, Asasi za Kiraia (AZAKI), na Nchi Wanachama ili kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kwa kuendana na mbinu za kazi zilizoanzishwa, ikiwemo kupitia Mikutano ya Kawaida ya umma ya kila baada ya miaka miwili.

vi. Kuhakikisha mbinu zake za kazi zinaongozwa na Waafrika na zinakuza mazingira chanya zaidi na yanayojikita kwenye uaminifu;

vii. Kushughulikia mitazamo inayohusiana na mamlaka yake ili kuongeza mwonekano wake, ufikiaji na kufaa kwake kama chombo cha kanda cha haki za binadamu;

viii. Kufanya mapitio ya Miradi yake Mikubwa ambayo inahitaji msaada wa kisiasa kutoka PRC na kuainisha masuala makuu yanayohusiana na masuala ya kiutamaduni na kisheria au mambo yoyote ambayo yanaweza kuleta ubishani au changamoto katika utekelezaji;

ix. Kuwasilisha vizuri mahitaji yake, maelezo ya bajeti, na changamoto zilizojitokeza kuimarisha msaada kwa kazi yake na kuwezesha ukusanyaji wa rasilimali;

x. Kuipa PRC uchanganuzi wa pengo la ufadhili wa bajeti, ukionesha tofauti kati ya bajeti iliyotengwa na mahitaji ya bajeti inayohitajika (Kiambatisho cha 2);

xi. Kueleza kwa ufasaha bajeti inayohitajika kwa ajili ya Miradi Mikubwa ili kuwezesha Kamati Ndogo ya PRC inayohusu Masuala ya Bajeti kutoa msaada pale inapolazimu;

xii. Kushirikiana na Kurugenzi ya Fedha ya AUC kuchunguza mbinu za ufadhili bunifu ambazo zitashughulikia changamoto za fedha, ikiwemo uainishaji wa vipengele vya bajeti;

xiii. Kuhakikisha upangaji bajeti halisi zaidi na unaotosha kwa ajili ya jumbe maalumu za ukuzaji kufikia malengo na mawanda ya kazi maalumu;

xiv. Kufanya mapitio ya kina ya mbinu za kazi zinazotumiwa na ACHPR kwa sasa katika kazi maalumu za ukuzaji ili kupima ubora wake katika kufikia matokeo yanayotakiwa huku yakiainishwa maeneno ya kuboreshwa;

xv. Kuendeleza na kuandaa mafunzo kwa Nchi wanachama, AZAKI zilizoidhinishwa, na wadau husika kuhusu kazi maalumu za ukuzaji za ACHPR ili kuongeza ufahamu na kuimarisha uelewa wa lengo na umuhimu wa kazi maalumu za ukuzaji;

xvi. Kufanya kazi za ukuzaji mara kwa mara kwa Nchi Wanachama ili kuleta ufahamu wa ACHPR, Mkataba wa Afrika, na vyombo vingine vya haki za binadamu;

xvii. Kuzingatia kupitisha chombo kinachofanana na APRM ambacho kinatoa mchakato uliopangwa na uliofafanuliwa vizuri wa kufanya kazi maalumu za ukuzaji ili kuhakikisha uidhinishaji wa kazi maalumu kwa wakati, ikiwa ni pamoja na miongozo na vigezo vilivyo wazi kwa ajili ya uteuzi na utoaji kipaumbele;

xviii. Kuomba Kitengo cha Mageuzi kutoa Ripoti iliyosasishwa ya mageuzi ya Vyombo na Taasisi za AU ili kuwezesha ACHPR kuandaa pendekezo lake na jibu na kuwasilisha kwa PRC;

xix. Kutoa nyaraka ya kina ya muundo yenye mpango wa gharama na wa utekelezaji (tazama Kiambatisho cha 3);

xx. Kutoa jedwali la kina la bajeti la mgao wa fedha uliopita na wa sasa na matumizi ya uendeshaji na ya programu, na takwimu zilizo wazi kuhusu pengo la fedha;

xxi. Kuweka vipaumbele vya wazi ili kuimarisha viwango vya utekelezaji wa kifedha na kiufundi kwa mujibu wa hatua za sasa ili kufanikisha matokeo mazuri na utekelezaji wa mamlaka yake;

xxii. Kuimarisha utekelezaji wa aina zote za mapendekezo ya ukaguzi (uchambuzi wa nje, wa ndani na wa kiuchunguzi) kuruhusu ongezeko la taratibu katika bajeti wakati wa mzunguko ujao wa bajeti;

xxiii. Kuimarisha ushirikiano wa mara kwa mara na Kamati ndogo za PRC, hususan Kamati ndogo ya PRC ya GSCBFAM kupitia Kamati ya Ushauri kuhusu Masuala ya bajeti na Wafanyakazi ya ACHPR, ili kuhakikisha kuna uelewa wa mahitaji na mapengo ya kifedha na kuruhusu msaada zaidi wa fedha;

xxiv. Kupanga upya mikutano ya wadau chini ya bajeti ya programu ili kuepuka kupunguzwa kwa bajeti;

xxv. Kuendelea kuongeza ufahamu wa Nchi Wanachama na kuwapa taarifa juu ya mamlaka na kazi za ACHPR;

xxvi. Kufanya shughuli za pamoja na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG ili kuimarisha ushirikiano;

xxvii. Kushiriki kwenye Kikao Kazi cha Bajeti kilichoitishwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa AUC;

xxviii. Kuchunguza uwezekano wa ufadhili kutoka kwa wadau wa Afrika ili kufadhili baadhi ya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za fedha za AU;

xxix. Kushirikiana na Sekretarieti ya AGA-APSA kuandaa Mpango wa ushirikiano na uhusiano kati ya ACHPR na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG katika kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu ndani ya Bara.

17. Kikao kazi cha pamoja kilipitisha **Mapendekezo Mahsusi yafuatayo kwa ajili ya hatua ya haraka:**

i. Kuazima Wafanyakazi kwenye ACHPR, hususan Kitengo chake cha Fedha na idara ya Manunuzi, kuziba pengo katika kazi za Fedha na Manunuzi, pamoja na Vitengo vya Usajili na Itifaki, ambavyo vinasimamiwa na mfanyakazi mmoja kila kimoja;

ii. Kuongeza mgao wa bajeti yake ya 2024 ili kuhudumia Mikutano miwili na kufanya kazi maalumu za ukuzaji zilizoidhinishwa na

iii. Kusaidia utekelezaji wa programu na miradi yake mikubwa na muhimu iliyoambatishwa kama **Kiambatisho cha 4**.

TAARIFA ZA WAJUMBE WA JUKWAA LA UTAWALA WA AFRIKA

ACHPR - MIPANGO YA UTETEZI KWA AJILI YA URIDHIAJI WA ITIFAKI KUHUSU HAKI ZA WAZEE NA HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU BARANI AFRIKA

18. Bi. Abiola, Kaimu Katibu Mtendaji wa ACHPR, alitoa taarifa kwa Kamati Ndogo juu ya mipango ya utetezi ya ACHPR kwa ajili ya Uridhiaji wa Itifaki kuhusu Haki za Wazee, na Haki za Watu Wenye Ulemavu barani Afrika, ambazo zinakamilisha Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu.

19. Taarifa iligusia hali ya utiaji saini na uridhiaji wa itifaki zilizotajwa hapo juu; iliangazia mipango mbalimbali ya utetezi ya Tume ya Banjul ya kukuza uridhiaji wa Itifaki hizo, na mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa. Mchango wake pia ulijikita kwenye nini kifanyike, hususan katika kuvuta umakini kwenye msaada ambao Kamati ndogo na PRC kwa ujumla ingeweza kutoa kwenye mipango hii ili kuhamasisha kuongezeka kwa uridhiaji wa Itifaki na kuharakisha kuanza kutekelezwa kwa itifaki hizo.

20. Wajumbe walikubaliana na kilichowasilishwa na kujadili umuhimu wa itifaki hizi. Pia waliomba kufanyike utafiti wa kina kuhusu kwanini Nchi Wanachama hawaridhii itifaki hizi. Pia walibainisha kuwa wakati wa kuridhia Nchi Wanachama wanapaswa kuzingatia hatua zinazofuatia ambazo watahitaji kuzichukua ili kuingiza kwenye mipango ya ndani, kutekeleza na kutoa ripoti kuhusu itifaki hizi.

ECOSOCC – MIPANGO YA ECOSOCC INAYOENDANA NA DEMOKRASIA, UTAWALA NA HAKI ZA BINADAMU

21. Bw. Kyeretwie Osei, Mkuu wa Programu wa ECOSOCC, alisisitiza kazi ya ECOSOCC katika kutangaza vyombo mbalimbali vya AU, pamoja na kuhamasisha wataalamu kutoka nchi mbalimbali kusaidia kazi ya taasisi mbalimbali kama vile Kamati Ndogo na PSC, na kusaidia asasi za kiraia kuwa bora zaidi katika kazi yao.

22. Mkuu huyo alitaja baadhi ya shughuli kubwa ambazo zimetekelezwa na kupangiliwa kama ifuatavyo: Jukwaa la Wananchi lilijikita kwenye masuala ya Mabadiliko yasiyo ya Kikatiba ya Serikali (UCGs), demokrasia, na utawala wa kidigitali; ushiriki wa asasi za kiraia katika kazi ya Jukwaa la Utawala wa Afrika (AGP); mradi unaoendelea unaoitwa *African Peoples Assembly,* ambao utatoa fursa kwa wananchi kutoka barani kote kuja na kubadilishana uzoefu wao kuhusu namna gani wanaishi katika hali ya maeneo yao kwa maana ya utawala wa kidemokrasia na utawala wa sheria; na uzinduzi wa Ripoti ya Hali ya Asasi za Kiraia katika mwaka ujao.

23. Wajumbe walipongeza wasilisho na kazi ambayo inafanywa na ECOSOCC na kuhimiza AZAKI na AU kufanya kazi kwa pamoja ndani ya mfumo wa ECOSOCC. Wajumbe pia walikubaliana kuwa ECOSOCC ni chombo ambacho kinahitaji kusaidiwa kupitia rasilimali na ufadhili.

TAARIFA YA KITENGO CHA KATIBA NA UTAWALA WA SHERIA CHA IDARA YA AUC-PAPS KUHUSU MKAKATI WA AU WA UJUMUISHAJI NA UINGIZAJI WA ACDEG KWENYE MTALAA WA SHULE

24. Bi. Abibata Barry, akiwakilisha kitengo, alitoa taarifa kwa Kamati ndogo kuhusu Mkakati wa AU wa ujumuishaji na uingizaji wa ACDEG kwenye mtalaa wa shule, kwa kurejelea mamlaka na malengo; awamu za Mradi; hali ya Mradi; nini kifanyike; na mapendekezo.

25. Wajumbe walipongeza wasilisho na kusisitiza umuhimu wa utekelezaji wa programu hii ili kuchangia kwenye uzuiaji wa migogoro. Kitengo kilitoa wito kwa Nchi Wanachama kusaidia mradi huu kwa kutoa mrejesho kuhusu nyaraka iliyotolewa kupitia balozi zao husika.

RIPOTI YA MWENYEKITI ANAYEMALIZA MUDA WAKE WA JUKWAA LA UTAWALA WA AFRIKA KUHUSU MAFANIKIO YA JUKWAA LA UTAWALA WA AFRIKA (AGP)

26. Katika taarifa yake kama Mwenyekiti wa AGP katika Ngazi ya Kifundi, Bi.Abiola Idowu Ojo, alisema kuwa Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jukwaa mnamo Oktoba 2021, kwa mujibu wa Ibara ya 6 ya Kanuni za Utaratibu za AGP. Mwenyekiti huyo alitoa taarifa fupi juu ya baadhi ya mafanikio, changamoto, na fursa za AGP.

27. Wakati wa uongozi wa ACHPR kuanzia 2021-2023, Mwenyekiti alionesha kuwa AGP imeitisha mikutano yake ya wadau inayofanyika kila baada ya miaka miwili katika ngazi zote mbili za kiufundi na kisiasa; ilifanya Tafakari muhimu ya Kimkakati kwenye

Jukwaa la sera na utoaji maamuzi na ilisaidia mkutano mmoja maalum wa AGP kwa ombi la Wajumbe.

28. Mwenyekiti huyo aliitaja AGP kuwa ni jukwaa pekee lililopo ambalo linaleta pamoja AU na RECs kwenye masuala ya utawala wa kidemokrasia na ni chombo cha kitaasisi na kiushirikiano cha Muundo wa Utawala wa Afrika (AGA) ambacho ni muundo wa kawaida unaotokana na maadili ya pamoja ya AU.

29. Mbali ya kuwapa wajumbe fursa ya kupanga kwa pamoja kwa ajili ya shughuli kubwa na kutekeleza kwa pamoja ni urasimishaji wa mikutano ya wadau ambayo itafanyika kando ya Mkutano Mkuu wa AU. Mikutano hii ni muhimu si tu katika kubadilishana uzoefu miongoni mwa wajumbe wa Jukwaa kulikopelekea mafanikio makubwa kwa mwaka kama mipango mikubwa ya AGP ambayo inajumuisha Ripoti ya Utawala wa Afrika, ambayo ni mpango wa Jukwaa, uandaaji wa Mazungumzo ya 12 ya Ngazi ya Juu (HLD), na Maadhimisho ya pamoja ya Siku ya Haki za Binadamu na mengine mengi.

30. Mwenyekiti alisema kuwa tangu kuungana kwa idara hizo mbili na kuwa moja - Idara ya Masuala ya Siasa na Amani na Usalama (PAPS) mnamo Machi 2021; Sekretarieti ya AGA ambayo ilikuwa muundo usio rasmi imerasimishwa kwenye muundo mpya wa AUC chini ya Kurugenzi ya Utawala na Uzuiaji wa Migogoro (GCPD) ndani ya PAPS.

31. Jambo hili ni mafanikio makubwa ya Jukwaa kwa vile Sekretarieti ya AGA inatumika kama Sekretarieti ya Jukwaa. AUC na idara hiyo zilionesha umuhimu wa ushirikiano kati ya vyombo vya utawala na vyombo vya amani na usalama na zilibadili Sekretarieti ya AGA kuwa Sekretarieti ya AGA-APSA ambayo ni ushuhuda wa kujitolea kwa kazi ya Jukwaa.

32. Kama mafanikio makubwa zaidi mpaka sasa, Kamati hii Ndogo inapaswa kuwa na ushirikiano rasmi na PSC. Kwa kuhusisha PSC Mwenyekiti alisema kuwa inaweza kuziba pengo kati ya utawala wa kidemokrasia, haki za binadamu, na amani na usalama.

33. Mwenyekiti pia alisisitiza kuwa mkutano wa mwaka wa AGP na PSC pia ulirasimishwa kufanyika kila mwaka na alishukuru kwa msaada wa chombo hiki cha Agosti kwenye suala hili. Kama maendeleo makubwa ya Jukwaa, Mwenyekiti alishukuru AGP kuja mbele ya PSC kama kundi kwa mara ya kwanza mnamo Agosti 2022 na kusherehekea ukweli kuwa mpaka sasa mikutano miwili ya kila mwaka imefanyika kati ya AGP na PSC wakati wa Uongozi wa ACHPR mwaka 2022 na 2023. Taarifa ya PSC ilitolewa kwa vyombo vyote viwili.

34. Bi. Abiola alifunga taarifa yake kwa kusistiza kuwa AGP ni chombo pekee kilichopo ambacho kinaleta pamoja watendaji wote wa haki za binadamu, utawala wa kidemokrasia katika sehemu moja ambacho kinajumuisha vyombo na RECs na kutaja kuwa hatuna chombo kama hicho. Ingawa Mageuzi ya AU yanatoa fursa kubwa kwa AGP na PAPS kwa kurasimisha Sekretarieti ya AGA-APSA chini ya Mageuzi ya AU, ambapo Sekretarieti

ya AGA-APSA kiukweli ingeweza kuimarisha Ushirikiano kati ya AGA na APSA na kuchangia ipasavyo kwenye ajenda ya utawala, uzuiaji wa migogoro, na ulinzi wa amani ndani ya Bara.

35. Mwenyekiti alitoa wito kuhusu ukweli kuwa haki za binadamu, utawala wa kidemokrasia ni muhimu katika kuendelea kwa amani na usalama na kwamba msaada wa kutosha unahitajika kutolewa kwenye ushirikiano kati ya miundo ya AGA na APSA kama kiwezeshi kikuu cha amani ya kudumu ndani ya Bara.

36. Mwenyekiti wa muda na Wajumbe wa Kamati Ndogo ya PRC walipongeza wasilisho hilo na kutambua umuhimu wa AGP katika kufanya kazi ya kukuza haki za binadamu barani Afrika. Kwa kutambua nafasi pekee ya jukwaa, mwenyekiti wa muda alitoa wito kwa Nchi zote Wanachama kuunganisha msaada wao kwa Jukwaa la Utawala wa Afrika na Sekretarieti.

KIAMBATISHO

- Mpango Kazi uliopitishwa wa mwaka 2023 wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG
- Hotuba ya Matokeo ya Kikao Kazi cha Pamoja kilichofanyika kati ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na ACHPR.

RASIMU YA UAMUZI JUU YA RIPOTI YA SHUGHULI ZA KAMATI NDOGO KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, DEMOKRASIA NA UTAWALA (HRDG)

Baraza Kuu,

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli za Kamati Ndogo kuhusu Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala (HRDG) kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2023;

2. **LINAIPONGEZA** Kamati Ndogo kwa kuthibitisha Ripoti ya Utawala wa Afrika ya mwaka 2023, ambayo iliandaliwa na APRM kwa niaba ya Jukwaa la Utawala wa Afrika (AGP) la Muundo wa Utawala wa Afrika (AGA);

3. **LINAKARIBISHA** muendelezo wa kikao cha mwaka cha pamoja kati ya Baraza la Amani na Usalama (PSC), Kamati ndogo ya PRC kuhusu HRDG na AGP na **LINASISITIZA** utekelezaji wa Taarifa ya PSC ya Mkutano wa 1167 kwenye Kikao cha Pamoja kilichofanyika tarehe 11 Agosti 2023;

4. **LINAPONGEZA** kazi ya wajumbe wa Jukwaa la Utawala wa Afrika hususan ACHPR katika kukuza na kulinda haki za binadamu na watu katika Bara na linatoa wito wa kuwa na uridhiaji wa pamoja wa Itifaki zinazohusiana. **LINAPONGEZA ZAIDI** kazi ya ECOSOCC kwa kushirikisha vizuri raia wa Afrika na Asasi za Kiraia katika masuala ya Umoja wa Afrika na **LINAONESHA** Kuunga mkono maandalizi ya Ripoti ya Hali ya Asasi za Kiraia Afrika (*African State of Civil Society Report)* ya mwaka 2024

5. **LINAZINGATIA** Kikao Kazi cha Pamoja kilichofanyika kati ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na ACHPR na linahimiza kuendelea kwa mashauriano haya ya pamoja na **LINATOA WITO** wa kuwa na msaada zaidi wa kisisasa, kifedha na kiuwezo kwa Vyombo vya AU vyenye mamlaka ya haki ya binadamu;

6. **LINAZINGATIA** kazi ya Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (PAPS) kuhusu hali ya Mkakati wa AU wa kujumuisha ACDEG kwenye mtalaa wa Shule na **LINATOA WITO** kwa Nchi zote Wanachama kusaidia mradi huu;

7. **LINATAMBUA** nafasi ya kipekee ya Jukwaa la Utawala wa Afrika (AGP) kama jukwaa pekee lililopo ambalo linaleta pamoja Vyombo vya AU, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), Vyombo vya Kikanda vya Ulinzi wa Haki (RMs) kwenye masuala ya haki za binadamu, demokrasia na utawala;

8. **LINASISITIZA** mchango mkubwa za Jukwaa la Utawala wa Afrika katika kukuza utawala wa kidemokrasia, amani na usalama ndani ya Bara, pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya Muundo wa Amani na Usalama wa Afrika (APSA na Muundo wa Utawala wa Afrika (AGA) na **LINATOA WITO** wa kutoa msaada wa kutosha na ulio sawa kwa mifumo na miundo ya AGA na APSA kama viwezeshi vikuu vya kuwa na amani endelevu barani Afrika;

9. **LINASISITIZA** wito wa kuwa na uridhiaji, uingizaji kwenye mipango ya ndani, utekelezaji na utoaji ripoti wa wote wa Vyombo vyote vya AU vya Maadili ya Pamoja, hususan Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Chaguzi na Utawala (ACDEG);

10. **LINATOA WITO** kwa Tume ya AU kuharakisha uendeshaji wa Kituo cha Utawala wa Afrika (*African Governance Facility)*;

11. **LINASISITIZA** ombi lililotolewa na PSC kwenye mkutano wa 1167 uliofanyika tarehe 11 Agosti 2023 kwa Tume ya AU kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Sekretarieti ya AGA-APSA ili kusaidia vizuri Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na Jukwaa la Utawala wa Afrika katika kutekeleza majukumu yao husika na **LINATOA WITO** wa kuwa na ushirikiano imara na ukamilishano wa jitihada kati ya AGA na APSA;

12. **LINAIOMBA** Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG na AGP kufanya ziara za ukuzaji juu ya Vyombo vya AU vya Maadili ya Pamoja; na kushiriki zaidi katika diplomasia ya kuzuia migogoro na jitihada za usuluhishi za Umoja wa Afrika;

13. **LINAIOMBA ZAIDI** Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG kuendeleza ushirikiano wake na Vyombo na Taasisi za AU zenye mamlaka ya Haki za Binadamu na Utawala kwa lengo la kuimarisha uratibu na ushirikiano, hususan katika kuimarisha ushirikiano kati ya Muundo wa Utawala wa Afrika (AGA) na Muundo wa Amani na Usalama wa Afrika (APSA);

14. **LINAIDHINISHA** pendekezo lililotolewa la kutangaza mwaka 2025 kama “Mwaka wa Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala barani Afrika”.

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

Report of the Sub-Committee on Human Rights, Democracy and Governance (HRDG)

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10500

Downloaded from African Union Common Repository